

Public education
Discover a world of opportunities

NAMBA: KUSOMEA NYUMBANI

MAWAZO YA SHUGHULI ZA HESABU NYUMBANI

Kusoma pamoja

Vitabu ni njia rahisi na nzuri ya kuleta hesabu nyumbani. Unapoendelea kusoma, ongezeza furaha kwenye mchezo kwa kuuliza maswali kama vile : *Ni nani alikuwa wa pili kufika ? Ni watu wangapi wana nywele za rangi ya udongo? Ni nani mtu mrefu zaidi katika picha? na Tuko ukurasa gani?* Hesabu kurasa wakati unazigeuza.

Chakula na kupika

Uliza watoto wako kukusaidia kupima viungo kwa kutumia vijiko, miiko, vikombe robo, vikombe nusu na vikombe. Uliza watoto wako waangalie mda wa kupikiaau kuweka saa juu ya tanuri.

Wasaidie kusoma orodha ya chakula cha shule cha mchana na gharama za vitu mbalimbali. Waache wahesabu fedha inahiyotajika.

Wasaidie watoto wako kujua jinsi vyakula na vinywaji vinavyoweza kugawika sawa, kwa mfano gawanisha mikate ya sandwichi au matunda katika nusu na kusema:

- Nimekata hii katika vipande viwili sawa - nusu ni yako na nusu ni yangu. Andaa chakula pamoja na uliza maswali kama :**
- **Tunahitaji masahani na vikombe vingapi?**
 - **Nina uma tatu, tunahitaji zingine ngapi?**
 - **Kila mtu anahitaji sausages mbili, je tunazo za kutosha?**

Zungumza kuhusu masaa

wasaidie watoto wako kusoma saa zote mbili za kisasa na za zamani. Zungumza kuhusu masaa Kwa mfano: *Kipindi chako unachokipenda cha televisheni huanza saa gapi? na kipindi hicho kina kaa kwa muda mgani?* Andika siku ya michezo na nyakati kwenye kalenda. zungumza juu ya siku za wiki, miezi yote ya mwaka na majira. husiana na matukio ya siku za wiki, kwa mfano: *Siku ya Jumatatu tunaenda kucheza na na Jumatano una mafunzo ya magongo.*

Michezo

Michezo ni habari zinazohushisha hesabu na ni rahisi kuzungumzia. Uliza maswali kama vile: *Ni pointi ngapi zinazo takikana kupata mambao matatu? Timu inaongoza kwa mambao mangapi? Ni mchezaji mgani amefunga magoli mengi? na Unaafahamu ni mwanariadhamgani mwenye muda wa kukimbia kwa kasi zaidi?*

Unaweza:

- onyesha alama na mda inavyoonekana kwenye ubao wa matokeo
- zungumza matumizi ya jumuisho na jinsi alama vinavyohesabiwa kwenye ubao.



Department of
Education

Utapata zaidi
Kijitabu cha ukweli cha kusomea nyumbani
Kwenye elimu hapa: education.wa.edu.au.